

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA ELIMU
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TUME YA NGUVU ZA ATOMU TANZANIA



UFADHILI WA SAMIA (SAMIA SCHOLARSHIP);
SHAHADA ZA UZAMILI (MSc) KATIKA SAYANSI NA
TEKNOLOJIA YA NYUKLIA: 2024/2025

KUHUSU UFADHILI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza mpango wa kukuza fani za Sayansi, Teknolojia, Ubunifu, Uhandisi, Hisabati na Tiba kupitia programu ya Ufadhili wa Samia (Samia Scholarship Extended Program).

Wizara kupitia Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC) inawatangazia Watanzania wenye Sifa kuomba ufadhili wa masomo ya Shahada za Juu (Uzamili) kwa wahitimu wenye ufaulu wa juu zaidi kwenye masomo ya sayansi kutoka katika vyuo vikuu vya Tanzania.

NCHI ZINAZOLENGWA

Ufadhili utatolewa kwa waombaji wenye udahili na ambao wanategemea kuomba au kupata udahili katika vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwenye nchi zifuatazo: Australia, Austria, Ubelgiji, Kanada, China, Jamhuri ya Cheki, Finlandi, Ufaransa, India, Swideni, Korea ya Kusini, Urusi, Uturuki, Uingereza na Marekani.

MAENEO YA UFADHILI

- 1.** Sayansi na teknolojia ya nyuklia katika matibabu ya saratani (medical physics, nuclear medicine)
- 2.** Sayansi na teknolojia ya nyuklia katika utafiti wa maji, hewa na mimea (isotope hydrology, space/airborne technology)
- 3.** Sayansi na teknolojia ya nyuklia katika unururishaji wa vifaa tiba, bidhaa za viwandani na mazao.
- 4.** Sayansi na teknolojia ya nyuklia katika nishati ya nyuklia na utafiti wa vinu vya nyuklia na uzalishaji wa dawa za mionzi.

SIFA ZA MWOMBAJI


- 1.** Awe Mtanzania mwenye umri usiozidi miaka 35;
- 2.** Awe mhitimu wa Chuo Kikuu katika shahada ya awali aliyemaliza katika kipindi kisichozidi miaka mitano kabla ya kuomba ufadhili huu.
- 3.** Awe na ufaulu wa juu wa kuanzia kiwango cha GPA ya 3.5 kati ya 5 au wastani wa ufaulu wa B kwa shahada ambazo hazina GPA kwenye matokeo ya jumla katika shahada ya awali ya sayansi, uhandisi, hisabati, tiba, tehama, mazingira, kilimo, na nishati pamoja na fani nyingine za vipaumbele vya Taifa;

NAMNA YA KUOMBA

Muombaji anapaswa kujaza fomu maalumu inayopatikana katika mtandao wa TAEC kupitia kiunganishi hiki <http://samiascholarship.taec.go.tz>

AU

Skani kodi ifuatayo na utembelee tovuti husika kwa ajili ya kufanya maombi.



MWISHO WA MAOMBI NI 15 AGOSTI 2024